# TARGETER WINGS
# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT
# GREDI YA SABA - 2024

Wings 005

# KISWAHILI

**Muda: Saa 1 dakika 20**

***Maagizo:***

***(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.***

***(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.***

**Jina** ______________________________

**Shule** ______________________________

**Nambari ya Usajili:** ______________ **Tarehe** ______________

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| **Swali** | **Upeo wa alama** | **Alama ya mwanafunzi** | **Kiwango cha utendaji** |
| **1 - 29** | **Alama 50** | | |
| **Jumla** | **50** | | |

**1. UFAHAMU WA KUSOMA**

**I *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 4*.**



Zamani katika kijiji cha Sanda paliishi sonara mmoja. Alikuwa na mke mrembo ambaye alihusudiwa na walimwengu wote wa eneo hilo. Karibu na nyumba yao kulikuwa na msitu ambao ulisetiri mazimwi ya kila aina. Kila jioni angeyasikia mazimwi hayo yaking'ang'ania mawindo. Sonara na mkewe walishangazwa jinsi viumbe hao walivyokithiri kwa tamaa.

Siku moja sonara alienda mji wa mbali kwa shughuli zake za ufuaji. Alimwacha mkewe akiwa na ujauzito. Saa chache baada ya kuondoka, uchungu wa uzazi ulibisha hodi.Mama mtu hakuwa na yeyote karibu wa kumsaidia. Ghafla bin vuu katika ile hali ya mahangaiko, akatokea mkunga mzuri na mpole ajabu. Mama akafurahi sana.

Baada ya hekaheka za hapa na pale mama akajifungua kitoto kichanga salama salimini. Akamshukuru mkunga kwa usamaria wema. Laiti angalijua kuwa amejibebesha mzigo usiobebeka! Mkunga hakukawia, aliingia ghalani akachukua mtama, akasaga na kumpikia uji. Mama hakuwa amepata hata nguvu ya kula. Alipotaka kukataa, alisikia sauti ikisema, "usipounywa mimi nitaunywa" sauti ilitisha. Mama aliposikia sauti hiyo, nywele zilimsimama kwa woga.

Jioni ilipofika njaa ilikuwa imemkabili mama. Yule mkunga zimwi akajigeuza binadamu akamchinjia kondoo mama mzazi. Lakini kabla ya kumpa, alirudia sauti ile ile, "ukikataa mimi nitamla kondoo mzima. Kondoo mzima akapata makao tumboni mwa zimwi. Siku tatu baadaye mama hakuwa ametia kitu tumboni. Unyoge wa uzazi ukamvamia. Kitoto kikaaga dunia.

1. Ni jambo gani lililoshangaza sonara na mkewe katika makazi yao?

2. Ni jambo gani ambalo linaonyesha kuwa sonara hakumjali mke wake kulingana na masimulizi?

3. Unadhani mtoto mchanga aliaga kutokana na shida gani?

4. **Andika maana ya:** 'Saa chache baada ya kuondoka, uchungu wa uzazi ulibisha hodi' ni

II. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 5 hadi la 8.***

Hakika, njia ni nyingi za kujiendeleza na kujinufaisha kiuchumi. Walio katika umri wa kujinufaisha na kujitafutia riziki ya kila siku, afua ni mbili: Uajiriwe au ujiajiri. Haya mambo mawili yamezua mjadala mkubwa duniani tangu zamani. Je, kujiajiri na kuajiriwa ni kupi kuliko na manufaa?

Sio siri kuwa kujiajiri kuna faida kubwa zaidi kuliko kuajiriwa. Ni furaha kubwa kuona mtu anayetumia maarifa, ujuzi na tajriba yake kuanzisha kazi au biashara yake mwenyewe. Wewe ndiwe bosi wako mwenyewe. Hupewi masharti na yeyote. Unajipa masharti wewe mwenyewe. Unajipangia malengo yako mwenyewe mradi kazi au biashara yako inazidi kunawiri. Uamuzi huwa ni wako. Kwa hivyo utafanya juhudi kuhakikisha kuwa malengo yako yameafikiwa.

Katika kazi za kujiajiri ni wewe binafsi unayetoa mipango na mikakati ya kufuata. Una maono na malengo ya muda mrefu na mfupi. Unajua ni wakati gani unahitaji mkopo au mtaji wa kupanulia biashara. Biashara inaponawiri, faida yote huwa ni yako.

Katika kazi za kujiajiri, hungoji hadi mwisho wa mwezi ndipo ulipwe mshahara kama zilivyo kazi za kuajiriwa. Pesa zipo na la muhimu ni wewe kupanga namna ya kuzitumia. Hakuna anayekunyanyasa au kujiingiza katika migogoro na mwajiri wako. Kazi za kujiajiri zinampa mtu ari na uwezo wa kujipima kusimamia biashara au kutunza mali. Mtu huyo pia anaweza kujiangalia na kujifunza kutokana na upungufu wake ikiwa utakuwepo.

5. Ni jambo gani ambalo limezua mjadala kulingana na kifungu?

6. Jambo lililo wazi kulingana na kifungu hiki ni lipi?
   A. Biashara haina faida kubwa kuliko kuajiriwa.
   B. Kujiajiri kuna faida kubwa kuliko kuajiriwa.
   C. Kazi za kujiajiri hazina malengo makubwa.
   D. Kuajiriwa kuna faida kuliko kujiajiri.

7. Pesa anazolipwa mtu aliyeajiriwa kila mwisho wa mwezi huitwaje?

8. Kulingana na kifungu, mtu anayejiajiri ana manufaa mengi sana. Unadhani ni hasara gani inayoweza kumpata anayejiajiri?
   A. Faida zote katika biashara huwa ni zake.
   B. Nafasi kubwa ya kujipatia utajiri na umaarufu.
   C. Hangoji hadi mwisho wa mwezi ili alipwe.
   D. Anaweza kufanya uamuzi mbaya ambayo inaweza kuathiri kazi au biashara yake.

## 2. UFUPISHO

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 9 hadi 12.***

Mungu alituumbia mazingira mazuri yasiyo na kasoro. Misitu kadhaa ya kusawazisha viwango vya oksijeni, maji safi yatiririkayo kutoka milimani, ardhi yenye rutuba, sehemu tambarare zinazovutia, wanyama wa kila aina na mambo mengine mengi.

Kwa sasa picha ni tofauti kabisa. Baadhi ya mandhari ni ya kutamausha. Sisi tulio na akili timamu tumevuruga usawa huu kwa sababu ya ulafi wetu wa starehe na mali. Kuharibu huku kwa mazingira ni sawa na kujiua. Hatima yake ni moja tu: Mauti.

Tumeishambulia misitu bila kujali. Tumeikata miti kiholela, na kuwapokonya wanyama makazi na lishe yao kwa kuwa kulikokuwa nyasi sasa ni mashamba.Sasa tunalia kuwa mwiba tuliojidunga sisi wenyewe.

9. Andika kichwa kinachofaa kifungu hiki?

10. Andika habari kuu inayojitokeza katika aya ya pili kwa sentensi moja.



CamScanner

11.Andika ujumbe wa aya ya tatu kwa maneno yaliyozidi 8.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

12.Andika habari muhimu inayojitokeza katika aya ya kwanza kwa sentensi moja.

______________________________________________

## 3. SARUFI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 13 hadi 17. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Raia wema hawapendi jinsi __13__ hisia __14__ kikabila __15__ miongoni mwa viongozi wetu. Ikumbukwe vyema kuwa kukabiliana na hisia ni jukumu la kila mmoja wetu. Iwapo tunatangamana katika shughuli zetu zote __16__ mbona basi __17__ saratani hii?

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13.A. ambapo | B. ambayo | C. ambazo | D. ambavyo |
| 14. A. ya | B. za | C.cha | D. wa |
| 15. A. zanakita | B. zajikita | C. zinavyojikita | D. zikijita |
| 16.A. , | B. ! | C. ; | D. : |
| 17.A. tutaendeleza | B. tunaendeleza | C. tunaendelesha | D. tumendelezea |

***Kuanzia swali la 18 hadi la 27, jibu swali kulingana na maagizo.***

18. ***Jaza nafasi kwa kutumia nomino sahihi ya makundi:***

Tina alijiandaa kufua __________ la nguo chafu.

19. Nomino, **'marashi na maarifa'** zinapatikana katika ngeli gani?

______________________________________________

20. ***Tambua aina ya neno lililopigiwa mstari katika sentensi:***

Sentensi: Nyanya anahisi <u>**maumivu**</u> makali mwilini. ______________________

21. Sentensi: Mwalimu anatushauri namna ya kutunza mazingira ipo katika hali gani?

______________________________________________

22. Tunga sentensi ukitumia kitenzi kishirikishi **'yu'**.

______________________________________________

23. ***Andika wingi wa:***

Kipakatalishi kitatumiwa kuhifadhi insha ya mwanafunzi.

______________________________________________

24. Chagua nomino isiyopatikana katika ngeli ya **LI-YA** kutoka kwenye kadi hii.

| | |
|---|---|
| Jokofu | Jiwe |
| Ziwa | Jua |

25. ***Kinyume cha neno mchana ni usiku. Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia kinyume cha neno lililopigiwa mstari.***

Chumba hiki kina <u>giza</u>. ______________________________

26. ***Tumia kiulizi mahali panapofaa katika sentensi:***

Kaka yangu aliniuliza, "unapenda kula chakula gani"

27. ***Kamilisha methali:***

Kinga na kinga ndipo ______________________________



CamScanner

**4. Fasihi**

**28. *Soma wimbo ufuataao kisha ujibu maswali:***

Viongozi walisema
Turudi mashambani
Makonge kushughulikia
Mimea kupalilia
Tutie ghera ndugu
Tujifunge masombo
Udongo tutifue
Magugu tung'oe
Kilimo tuimarishe
Pasiwe wa kutuvuta
Misri kuturudisha
Kwa pato la kufutia chozi
Ukame tutwandama
Mashamba tukiachilia
Mmonyoko kuyatwaa
Tutabaki mikunguni
Kutegemea wahisani.

a) Wimbo huu huimbwa wakati wa kufanya kazi gani? (alama 1)

______________________________

b) Eleza sifa tatu za wimbo wa aina hii zinatojitokeza katika wimbo huu (alama 3)

______________________________

______________________________

______________________________

c) Taja majukumu matatu ya nyimbo za kazi yanayotekelezwa na wimbo huu. (alama 3)

______________________________

d) Kwa mujibu wa wimbo, ni nani anatoa wito kwa watu wafanye kazi. (alama 1)

______________________________

e) Ikiwa utawasilisha wimbo huu kwa wenzako darasani, taja mafunzo mawili watapata kutoka kwa wimbo huu. ______________________________ (alama 2)

**5. Dondoo**

**29. *Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.***

"Juzi nilishangaa sana kugundua kwamba Hidaya ana ujuzi wa tarakilishi. Tarakilishi kwa Kiingereza inaitwa "Computer." Tarakilishi ni kifaa cha kidijitali ambacho kimekuwa maarufu kila mahali ulimwenguni.

Kompyuta ilipovumbuliwa, kulizuka mgogoro mkubwa ulimwenguni. Kuna walioogopa kwamba itapokonya watu kazi. Usilolijua ni usiku wa giza. Sasa kuna kompyuta kila mahali. Kinyume na hofu ya akina yakhe waliozoea kufanya kazi ya sogi, watu wanaendelea kuajiriwa kila uchao," aliongeza mwalimu mkuu.

Alifafanua kwamba kutokana na tarakilishi, sasa kuna kitu kijulikanacho kama baruapepe, yaani "electronic mail" au kwa ufupi e-mail. Hii ni njia ambayo mtu anaweza kuwasiliana na mwenzake kupitia tarakilishi na kuandika barua yake.

Mwalimu mkuu alimpa Hidaya fursa awafafanulie wenzake jinsi tarakilishi inavyofanya kazi.

a) Andika mandhari ambayo yanajitokeza katika dondoo hili.

______________________________

b) Fafanua dhamira ya mwandishi katika dondoo hili.

______________________________

c) Mwenzako amesoma dondoo hili.Fafanua mafunzo matatu ambayo atapata.

______________________________

d) Mwandishi wa dondoo hili ametumia mbinu za lugha tofauti tofauti. Zitaje tatu.

______________________________



CamScanner

# TARGETER WINGS
# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

Wings 005

# GREDI YA SABA - 2024
## SEHEMU B:
## KISWAHILI : INSHA

*MUDA: Dakika 40*

| | |
|---|---|
| **Jina** ______________________________ | |
| **Shule** ______________________________ | |
| **Nambari ya Usajili:** ______________ | **Tarehe** ______________ |

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**

2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

© *Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd. Email:info@targeterpublishers.co.ke*

**FUNGUA KURASA**

CamScanner

*Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo:*

***Ilikuwa mara yangu ya kwanza kuzuru mbuga ya wanyama. Siku hiyo ...................***